JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
TAASISI YA UTAFITI WA MISITU TAANZANIA

# MAFANIKIO MUHIMU YA UTAFITI WA MISITU NA UFUGAJI NYUKI KWA KIPINDI CHA 2021 - 2025

Picha

**Machi, 2026**

## YALIYOMO

1

YALIYOMO ........ 2

1. UTANGULIZI ........ 3

1.1 Uanzishwaji wa TAFORI ........ 3

1.2 Dira na Dhima ........ 3

2. MAJUKUMU YA TAASISI ........ 4

3. MAFANIKIO YA UTAFITI KWA KIPINDI CHA 2021 MPAKA 2025 ........ 5

3.1 Miongozo Inayosimamia Utafiti ........ 5

3.2 Tafiti zilizofanyika ........ 5

3.2.1 Utafiti wa Afya ya Misitu washauri Mbinu za Utunzaji wa Mashamba ya Miti ya Serikali na Sekta Binafsi ........ 5

3.2.2 Utafiti wa Umri wa Uvunaji wa Miti ya Misindano na Misaji Wapunguza Muda wa Kuvuna ........ 6

3.2.3 Utafiti wa Ubora na Matumizi ya Mbao Washauri Miti ya Asili Isiyofahamika Sana Kuvunwa ........ 7

3.2.4 Utafiti Juu ya Moto wa Msituni Washauri Wadau Kuchukua Tahadhari ........ 7

3.2.5 Utafiti wa Sifa za Asali ya Tanzania Yawezesha Kutengeneza Alama ya Asali (Honey Trademark) yenye Usajili Namba TZ/T/2023/3136 ........ 8

3.2.6 Matumizi ya TEHAMA Yaongeza Ufanisi wa Utendaji Kazi ........ 8

3.2.7 Tafiti Juu ya Mimea Vamizi Zinawezesha Ufuatiliaji na Kujengwa Uwezo kwa Jamii ........ 9

3.2.8 Tathmini ya Rasilimali za Misitu Kuongeza Tija katika Viwanda vya Mazao ya Misitu Nchini ........ 10

3.2.9 Utafiti wa Ufugaji Nyuki Endelevu Kutatua Changamoto Zinazoikabili Sekta ili Kuboresha Maisha, Maendeleo ya Viwanda na Uhifadhi Wa Bioanuai ........ 11

3.2.10 Utafiti wa Nyuki Wasiodunga Wabaini Nyuki Wanaofaa Kufugwa Jirani na Makazi ........ 12

3.3 Usambazaji wa Matokeo ya Utafiti ........ 13

4.0 HITIMISHO ........ 15

# 1. UTANGULIZI

## 1.1 Uanzishwaji wa TAFORI

Utafiti wa misitu nchini Tanzania ulianza miaka ya 1890 wakati wa Serikali ya Kikoloni ya Wajerumani. Baada ya hapo, Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Kibaiolojia kilianzishwa huko Amani mnamo 1902 ili kuanzisha utafiti wa miti asilia na ya kigeni. Mwaka 1928, Serikali ya Kikoloni ya Uingereza ilibadilisha jina la Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Baiolojia cha Amani na kuwa Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Afrika Mashariki na kukihamishia Muguga (Kenya) na baadae mwaka 1948 kuunda Shirika la Utafiti wa Kilimo na Misitu la Afrika Mashariki ambalo lilihusika na tafiti zote za kilimo na misitu za Afrika Mashariki (Kikanda). Mwanzoni mwa miaka ya 1950, Serikali ya Tanganyika ya wakati huo ilianzisha Vituo vya Utafiti wa *Silvicultural* na *Utilization* huko Lushoto (Tanga) na Moshi (Kilimanjaro) mtawalia ili kukidhi tafiti mahususi za ndani ya nchi. Kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, ambayo ilikuwa mwavuli wa shirika lililokumbatia shughuli za utafiti wa kilimo na misitu za kikanda, kulisababisha kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) mwaka 1980. Hivyo, TAFORI imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Mwaka 1980 na Marejeo yake ya Mwaka 2023. Kupitia Sheria hiyo Taasisi ilipewa jukumu la kufanya, kusimamia, na kuratibu tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi ya teknolojia bora za uendelezaji wa misitu na ufugaji nyuki nchini. Taasisi kwa kwa kipindi cha 2021 – 2025 imefanikiwa kufanya tafiti za kimkakati mbalimbali, ambapo matokeo ya tafiti hizi yamesaidia kuimarisha maendeleo nchi na jamii kwa ujumla. Baadhi (10) ya tafiti hizi, zinaelezwa kwenye kitabu hiki.

## 1.2 Dira na Dhima

i) Dira ya Taasisi ni kuwa kitovu cha mafanikio ya utafiti wa misitu na ufugaji nyuki kwa maendeleo ya Tanzania.

ii) Dhima ya Taasisi ni kusaidia maendeleo ya misitu na ufugaji nyuki kupitia kufanya, kuratibu, kudhibiti utafiti na usambazaji ya matokeo.

## 2. MAJUKUMU YA TAASISI

Kifungu cha 4 (1) (a)-(s) cha Sheria iliyoanzisha TAFORI (Sheria Na. 5 ya mwaka 1980) na maboresho yake ya mwaka 2023 kimeainisha majukumu 16 ya Taasisi. Majukumu hayo yanajikita kutekeleza majukumu makuu yafuatayo;

(a) Kufanya na kuhamasisha kufanyika kwa utafiti wa misitu na ufugaji nyuki;

(b) Kuratibu tafiti za misitu na ufugaji nyuki ambazo zinafanyika ndani ya nchi;

(c) Kusambaza matokeo ya utafiti kwa wadau pamoja na kuanzisha na kuendesha mfumo wa utunzaji taarifa na usambazaji wa matokeo ya tafiti;

(d) Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu teknolojia bora, mbinu za uhifadhi, uzalishaji na matumizi ya mazao ya misitu na nyuki kwa Serikali, Taasisi za umma na wadau wengine;

(e) Kushirikiana na Serikali au Taasisi au wadau wengine, kuhamasisha, au kutoa nyenzo kwa ajili ya mafunzo na maelekezo kwa wazawa kufanya tafiti na usimamizi wa Rasilimali misitu na nyuki;

(f) Kutekeleza wajibu wa udhibiti na usimamizi wa rasilimali ambazo zimeanzishwa au kukabidhiwa kwa Taasisi chini ya kifungu cha 5 au sheria nyingine yoyote; na

(g) Kufanya au shughuli yoyote ambayo, kwa maoni ya Bodi, inalenga kuwezesha Taasisi kutekeleza majukumu chini ya Sheria iliyoanzisha.

## 3. MAFANIKIO YA UTAFITI KWA KIPINDI CHA 2021 MPAKA 2025

### 3.1 Miongozo Inayosimamia Utafiti

Utekelezaji unazingatia Mpango wa Taifa wa Watatu wa Utafiti wa Misitu (National Forestry Research Master Plan III (NAFORM III: 2021-2031); Mpango wa Taifa wa Kwanza wa Utafiti wa Ufugaji Nyuki (*National Beekeeping Research Master Plan I* (NABERM I: 2020-2030); na Mpango Mkakati wa Taasisi (2021/2022 -2025/2026)




**Kielelezo 1:** Miongozo ya tafiti zilizofanyika

Aidha miongozo mingine inayosimamia kufanya, kuratibu na kusambaza matokeo ya Utafiti ni Sheria ya TAFORI Na. 5 ya 1980 kama ilivyorejewa Mwaka 2023 na Kanuni zake za Mwaka 2020; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025; Sera ya Taifa ya Misitu (1998); Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998); Sheria ya Misitu Na.14 (2002) na Kanuni zake; Sheria ya Ufugaji Nyuki (2002) na Kanuni zake.

### 3.2 Tafiti zilizofanyika

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, Taasisi imetekeleza miradi hamsini na nane (58) ya utafiti wa misitu na sita (6) ya utafiti wa ufugaji nyuki. Matokeo ya tafiti yamewezesha maamuzi ya kisera, uandaaji wa miongozo, taarifa za kuwezesha ugani na mafunzo na kukuza na kuendeleza ubunifu na tekninolojia. Matokeo ya baadhi ya tafiti kubwa ni kama ifutavyo:

#### 3.2.1 Utafiti wa Afya ya Misitu washauri Mbinu za Utunzaji wa Mashamba ya Miti ya Serikali na Sekta Binafsi

Taasisi imefanya utafiti wa kubaini changamoto na kushauri juu ya afya ya miti katika mashamba ya Serikali na watu binafsi ili kupata mazao yaliyotarajiwa. Utafiti umebaini

kuwa matukio ya kukauka kwa miti katika mashamba ya miti yanasababishwa na uwepo wa magonjwa ya miti, wadudu waharibifu, kupanda miti kwenye maeneo yasiyo sahihi, kutotunza miti ipasavyo na mabadiliko ya tabia nchi.



**Kielelezo 2:** Miti iliyoshambuliwa na ugonjwa wa kukauka na kudumaa katika moja ya mashamba ya miti hapa nchini

Taasisi imeshauri namna mbalimbali za kudhibiti kufa/kukauka ambao umeisaidia wadau na wakulima wadogo katika Mikoa ya Iringa na Njombe kukabiliana na majanga ya wadudu waharibifu, magonjwa na changamoto nyinginezo zinazoikabili sekta ya misitu.

### 3.2.2 Utafiti wa Umri wa Uvunaji wa Miti ya Misindano na Misaji Wapunguza Muda wa Kuvuna

Utafiti umeonesha kuwa umri wa kuvuna miti aina ya misindao ni kuanzia miaka 18 na kuendelea kwa ajili ya matumizi ya mbao. Miti ya Misindano pia inaweza kuvunwa ikifikisha umri wa kuanzia miaka 11 kwa ajili ya uzalishaji wa karatasi. Miti ya misaji umri wa kuvuna ni miaka 20 na kuendelea kwa ajili ya matumizi ya mbao. Utafiti huu umesaidia Serikali na Watu binafsi kupata mapato mapema badala ya kusubiri miaka mingi zaidi kama ilivyozoeleka bila kuathiri ubora wa mazao. Aidha utafiti huu umeongeza makadirio ya ujazo wa miti inayovunwa kwa mwaka, kuongeza ajira, na kuwezesha kutengeneza Agizo la kiufundi Na.1 la 2021.

### 3.2.3 Utafiti wa Ubora na Matumizi ya Mbao Washauri Miti ya Asili Isiyofahamika Sana Kuvunwa

Utafiti uliofanyika kubaini ubora wa miti ya asili na kuipanga madaraja yake ya ubora. umesaidia kuboresha Tangazo la Serikali linalohusu tozo baada ya spishi 12 kati ya 19 iliyofanyiwa utafiti na kupangiwa madaraja husika katika jedwali Na. 8 la kanuni namba 627 ya mwaka 2020. Mabadiliko haya yameiongezea mapato Serikali baada ya kupandisha bei ya spishi 15 kutoka shilingi 145,000 hadi 350,000 kwa meta moja ya ujazo.

### 3.2.4 Utafiti Juu ya Moto wa Msituni Washauri Wadau Kuchukua Tahadhari

Taasisi imekusanya na kusambaza taarifa za moto wa msituni kwa kutumia “satellite”. Taarifa zinaonesha kuwa moto wa msituni bado ni changamoto kubwa kwa kuwa unaharibu rasilimali miti, bionuai, viota vya nyuki na mazingira ya utalii ikolojia. Katika kipindi cha mwaka 2023/24 eneo la misitu lililoathirika na moto ni kilometa za mraba 65,077.98 sawa na asilimia 6.92 ya eneo lote la Tanzania Bara. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2024/25 eneo la misitu lililoathirika na moto ni kilometa za mraba 80,526.05, sawa na asilimia 8.81 ya eneo lote la Tanzania Bara. Maeneo yaliyoathirika zaidi katika kipindi tajwa ni pamoja na Mikoa ya Lindi, Katavi, Morogoro, Mbeya, Tabora na Ruvuma. Matokeo ya utafiti yamesaidia Serikali na wadau wengine kuchukua tahadhari na majanga ya moto kwenye maeneo yenye misitu. Aidha, TAFORI kwa kushirikiana na wadau inaendelea kuelimisha umma mbinu za kuchukua tahadhari na kuzuia moto wa msituni.



**Kielelezo 3:** Mojawapo ya maeneo yaliyoathiriwa na moto wa misituni Nchini

### 3.2.5 Utafiti wa Sifa za Asali ya Tanzania Yawezesha Kutengeneza Alama ya Asali (Honey Trademark) yenye Usajili Namba TZ/T/2023/3136

Utafiti ulifanyika kuangalia sifa za asali inayozalishwa katika uoto mbalimbali hapa nchini Tanzania (mikoa, hali ya hewa, udongo, na vyanzo vya maua) kwa kuzingatia sifa za hisia, kemikali ya fizikia na *antimicrobial*. Matokeo ya utafiti huu yamewezesha kupatikana kwa Alama ya asali ya Tanzania yaani Tanzania Honey Mark inayosimamiwa na Mamlaka ya Biashara Tanzania (TANTRADE) ambayo ilizunduliwa na Mhe. Waziri wa Maliasili na Utalii Oktoba 2024 Mjini Tabora. Aidha, matokeo ya utafiti huu yamewezesha kutengeneza tovuti inayotoa taarifa za asali kulingana na uoto ya www.tanzaniahoney.org kwa lengo la kutangaza asali ya Tanzania katika masoko ya ndani na nje ya nchi.




**Kielelezo 4:** Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana akizindua Alama ya Asali, Mkoani Tabora

### 3.2.6 Matumizi ya TEHAMA Yaongeza Ufanisi wa Utendaji Kazi

Taasisi kwa kushirikiana na Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) imetengeneza mfumo wa Kielektroniki wa kusajili watafiti na tafiti, kutoa idhini ya utafiti, kuchapisha maandiko na kuweka kanzidata ya utafiti wa misitu na ufugaji nyuki. Mfumo huu unawawezesha watafiti wa misitu na nyuki kujisajili, kuandikisha miradi ya kitafiti, kupata vibali vya Utafiti, na kuwezesha Taasisi kuratibu utekelezaji wa utafiti unaofanywa na wadau nchini.

Tangu Mfumo huo uanzishwe mwaka 2022/2023, Taasisi imesajili mradi 46 (29 ya ndani na 17 kutoka nje) na kusajili Watafiti 163 wa kutoka ndani 120 na nje ya nchi 43 wanaotekeleza shughuli za kitafiti nchini.

### 3.2.7 Tafiti Juu ya Mimea Vamizi Zinawezesha Ufuatiliaji na Kujengwa Uwezo kwa Jamii

Taasisi kwa kushrikiana na wadau kutoka Uswisi inatekeleza mradi wa utafiti kudhibiti mimea vamizi kwenye maeneo ya wafugaji katika Wilaya ya Longido, Mkoa wa Arusha na Siha, Mkoa wa Kilimanjaro. Utafiti unawezesha urudishaji wa uoto wa asili katika maeneo yaliyovamiwa na mimea vamizi ambapo majaribio ya mbinu mbalimbali za kurudisha uoto wa asili yameanzishwa katika vijiji vya Tingatinga Wilaya ya Longido na Mawasiliano Wilaya ya Siha. Utafiti huu unasaidia kuimarisha ulinzi dhidi ya mimea vamizi ili isiende katika maeneo hifadhi za misitu na wanyamapori nchini. Kwa upande mwingine, TAFORI inashirikiana na Taasisi nyingine za Serikali na wataalam kutoka nchini Cuba kutathmini aina, mtawanyiko, athari na mbinu za udhibiti wa mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa. Matokeo ya awali yamebaini uwepo wa aina mbalimbali za mimea vamizi kama vile; *Gutenbergia cordifolia, Bidens schimperi, Parthenium hysterophorus, Verbena officinalis, Chromolaena odorata, Opuntia vulgaris, Datura stramonium, Parthenium hysterophorus, Eichhornia crassipes* (Water hyacinth), na Salvinia species. Kufuatia matokeo hayo, TAFORI inaendelea kushirikiana na watafiti wa ndani (TAWIRI na SUA) na nje ya nchi kubuni mbinu zitakazowezesha kudhibiti uvamizi wa mimea na kuenea katika maeneo ya hifadhi na vijiji ili isiathiri idadi ya watalii watarajiwa kwa mwaka.



**Kielelezo 5:** Mimea vamizi wilaya ya Longido, Mkoa wa Arusha



**Kielelezo 6:** Gugu karoti linaloathiri eneo la kreta katika Hifadhi ya Ngorongoro

### 3.2.8 Tathmini ya Rasilimali za Misitu Kuongeza Tija katika Viwanda vya Mazao ya Misitu Nchini

Taasisi imefanya tathimini ya rasilimali za misitu na uwepo na uwezo wa viwanda vya misitu nchini. Tathmini imeonyesha kuwa kuna misitu ya kupandwa kiasi cha hekta 303,668.05 ambapo asilimia 68 inapatikana Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. Pia, tathmini imeonesha uwepo wa viwanda vya msingi vya misitu 1,572 ambavyo vinatoa ajira kwa watu 17,192 katika makundi tofauti ya kijamii. Aidha, tathimini imebaini mahitaji ya malighafi kwa viwanda vya misitu vilivyopo ni mita za ujazo 7,172,596 kwa mwaka na kiwango kinachopatikana kwa mwaka ni mita za ujazo 2,155,976.00 sawa na asilimia 30 ya mahitaji. Matokeo haya yanatoa taswira halisi kuwa viwanda vingi vinafanya kazi chini ya uwezo kutokana na ufinyu wa malighafi na hivyo jitihada zinahitajika kuongeza kasi ya upandaji miti na hifadhi ya misitu asili.

**Kielelezo 7**: Viwanda vya uchakatiji wa mabao

### 3.2.9 Utafiti wa Ufugaji Nyuki Endelevu Kutatua Changamoto Zinazoikabili Sekta ili Kuboresha Maisha, Maendeleo ya Viwanda na Uhifadhi Wa Bioanuai

Lengo la utafiti ni kutoa majawabu ya changamoto zinazokabili sekta ndogo ya ufugaji nyuki ambazo ni uzalishaji mdogo, makundi ya nyuki kuhama, kutojua maeneo sahihi ya kufuga na kundi la vijana na wanawake kutokushiriki kwa dhana kuogopa kudungwa na nyuki.. Utafiti umebaini kuwa mizinga ya michi (Top Bar Hives) inakamata makundi ya nyuki kwa asilimia 73.1 ikilinganishwa na mizinga ya viunzi (Frame hives) yenye asilimia 39.7. Aidha, uzalishaji wa asali kwa mzinga unatofautiana kutoka eneo moja la uoto hadi jingine. Kwa mfano mzinga wa kati unaobeba michi 17 umezalisha kilo 12.9 kwa Wilaya ya Kasulu, kilo 18 Wilaya ya Butiama, Kilo 6 Rondo Lindi, kilo 21. 6 Wilaya ya Chamwino na kilo 18.7 Wilaya ya Kongwa. Aidha matokeo yanaonesha kuwa uzalishaji wa asali unategemea jamii ya nyuki anayedungwa aina ya *Apis meliffera scuttellata.* Ambaye anapatikana katika maeneo yote nchini. Utafiiti unashauri wafugaji kuwa uzalishaji kwa mzinga unachangiwa kwa kiasi kikubwa na kiwango cha mbochi kutoka mimea iliyopo, ukaribu wa maji katika eneo la kufuga nyuki, utundikaji sahihi wa mizinga na usimamizi wa manzuki na makundi ya nyuki.




**Kielelezo 8**: Mizinga ya Vihunzi katika Manzuki  ya majaribio Wilayani Kongwa

### 3.2.10 Utafiti wa Nyuki Wasiodunga Wabaini Nyuki Wanaofaa Kufugwa Jirani na Makazi

Taasisi inaratibu utafiti wa ufugaji wa nyuki wadogo ambao unajumuisha watafiti kutoka Taasisi sita ambazo ni TAFORI, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI), Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora (BTI), na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Utafiti wa awali umebaini kuwa spishi za nyuki wasiodunga katika Genera Hypotrigona (maeneo ya tambarare na mwambao ya bahari ya hindi na Axestotrigona maeneo mengine ndizo zinazofaa kufugwa katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya uzalishaji wa asali.  Utafiti pia umebaini uzalishaji wa asali kwa nyuki hawa unatofuatiana kulingana na hali ya hewa ya eneo husika. Mfano wastani wa uzito unaozalishwa kwenye maeneo tofauti  ni kilo 1.5 hadi 9.5. Aidha, utafiti unaendelea katika vibanda vya majaribio ya kufuga nyuki wasiodunga (meliponary shades) vilivyojengwa katika maeneo tisa (9) ya wilaya za Rufiji, Mkinga, Siha, Kondoa, Manyoni, Mpanda, Biharamulo, Mbeya na Magharibi ambayo yanawakilisha kanda nne za tabia nchi (climatic zones) nchini.




**Kielelezo 9:** Aina za nyuki wasiodunga na mizinga inayotumiwa na jamii

### 3.3 Usambazaji wa Matokeo ya Utafiti

Taasisi imesambaza matokeo ya utafiti kwa njia mbalimbali ambazo zimewezesha TAFORI kuwafikia wadau katika kueneza maarifa, kuongeza ufahamu katika utekelezaji wa sera za sekta ya misitu na ufugaji nyuki na kuchangia maendeleo endelevu ya Tanzania. Njia hizo ni:


i) Kuchapisha makala za kisayansi (scientific papers) 42 kutokana na tafiti zilizofanyika.
ii) Kuandaa na kusambaza toleo la Proceedings ya Kongamano la Pili na la Tatu la Kimataifa la Kisayansi kwa washiriki na wadau wa utafiti wa ndani na nje ya nchi.
iii) Kuandaa programu nne (4) za mafunzo juu ya uandishi na tafsiri ya matokeo ya utafiti,
iv) Kusambaza matokeo kumi (10) ya utafiti, kupitia vyombo mbalimbali vya habari (redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii), na
v) Kongamano la Kimataifa la Kisayansi. Taasisi iliandaa Makongamano mawili ya Kimataifa yaa Kisayansi. Kongamano la Pili la Kimataifa la Kisayansi lilifanyika Februari, 2021 Jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na washiriki 196. Aidha, Kongamano la Tatu la Kimataifa la Kisayansi lilifanyika mwezi Disemba, 2024 Jijini Arusha na kuhudhuriwa na Washiriki 996, kutoka Tanzania na Mataifa mbalimbali ikiwemo Kenya, Afrika Kusini, Uswisi, Japan, Estonia, Ufini na Ujerumani




**Kielelezo 11:** Washiriki wa Kongamano la Tatu la Kisanyansi la Kimataifa lilofanyika Disemba, 2024 Jijini Arusha.

## 4.0 HITIMISHO

Taasisi inaishukuru Serikali kwa kuwezesha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, bila kuwasahau Wadau mbalimbali ambao wameendelea kushirikiana na TAFORI kutimiza majukumu yake na hivyo kuiwezesha kufikia mafanikio iliyopata. Taasisi itaendelea kujikita zaidi katika kufanya tafiti za kisayansi zenye ubora, kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali, ili kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu na nyuki. Taasisi itahakikisha matokeo ya tafiti zake yanatumika kuongeza ufanisi wa sera za misitu na nyuki, kukuza uchumi endelevu kupitia faida za kijamii na kiuchumi, na kuchangia katika kuhifadhi mazingira kwa vizazi vya sasa na vijavyo.



**Kwa Mawasiliano:**

**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania**
**S. L. P 1854 | Morogoro | Tanzania**
**Simu: +255 23 2935174**
**Nukushi: +255 23 2935174**
**Barua pepe: tafori@tafori.or.tz**
**Tovuti: www.tafori.or.tz**